

SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA (TBS)



MFUMO WA ULIPAJI KWA NJIA YA KIELEKTRONIKI

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linapenda kuutarifu umma kuwa limejiunga kwenye mfumo wa Serikali wa malipo ya kielektroniki kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Fedha za Umma ya 2017 yanavyoelekeza kuwa fedha zote za umma zinapaswa kukusanywa kupitia mfumo wa serikali wa malipo ujulikanao kama *Government e-Payment Gateway* (GePG). Ili kwenda sanjari na mfumo wa Serikali, TBS imetengeneza mfumo wa malipo wa kielektroniki (Electronic Payment System, ePS) ambao umeunganishwa na mfumo wa serikali (GePG). Mfumo huu mpya wa malipo wa TBS (ePS) uliingizwa rasmi katika matumizi tarehe 10 Januari, 2018 kwa ofisi za TBS zilizoko Dar es Salaam.

Kwa sasa, njia pekee ya kufanya malipo yoyote kwa TBS kwa wateja wote wa ndani na nje ya nchi ni kwa kutumia mfumo huu mpya wa kielektroniki (ePS).

Njia za kulipia huduma kwa njia ya kielektroniki

1. Kwa njia ya kuweka Fedha Benki

Nenda kwenye tawi lolote la benki au wakala wa benki ya CRDB /NBC/ NMB kwa kutumia nambari maalumu (control number)

2. Kwa njia ya Mitandao ya Simu.

Tumia Airtel Money, Tigopesa, M-Pesa au Hallo Pesa kwa kutumia Nambari ya Kampuni 888999 na Kumbukumbu namba ya malipo

3. Kwa njia ya Kuhamisha Fedha

Unaweza kuhamisha fedha moja kwa moja kutoka katika benki yoyote kwenda kwenye akaunti zetu zilizoko katika Benki ya TBS ya NMB , CRDB , au NBC kwa njia ya TISS/SWIFT kwa kujaza: Namba ya Akaunti (Field 59) na Kumbukumbu namba ya Malipo (Field 70).

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

Mkurugenzi Mkuu

Shirika la Viwango Tanzania

S.L.P 9524

DAR ES SALAAM

Simu: +255 2450298

Nukushi: +255 22 2450959

Barua pepe: info@tbs.go.tz

Hotline: 0800110827